

Serikali kuchanja mifugo nchi nzima



Picha:IN



Picha:IN

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi mwaka huu wa 2025 itaendesha nchi nzima zoezi la uchanjaji wa Ng'ombe dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu (CBPP), Mbuzi na Kondoo dhidi ya Ugonjwa wa Sotoka (PPR) na Kuku dhidi ya Ugonjwa wa Mdondo/ Kideri (Newcastle disease)

Gharama ya chanjo kwa Ng'ombe mmoja ni shilingi mia tano (500/=), Mbuzi/Kondoo mmoja ni shilingi mia tatu (300/=). Kuku watachanjwa BURE

Katika zoezi hili la chanjo, majukumu ya mfugaji ni kama ifuatavyo:-

1. Kushiriki katika kuandaa eneo na

miundombinu ya kutolea huduma ya chanjo.

2. Kushirikiana na vyama vya wafugaji na viongozi wa vijiji au mitaa kuhamasisha umuhimu wa chanjo kwa wafugaji wengine katika zoezi la chanjo .
3. Kupeleka mifugo kwenye vituo vya chanjo kulingana na ratiba ya chanjo.
4. Kulipia gharama za chanjo kama inavyoelekezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ama uongozi wa Halmashauri kwa maeneo husika.
5. Kutunza daftari la kumbukumbu za chanjo zinazotolewa katika mifugo yake kwa lengo la kusaidia ufuatiliaji wa kiwango cha uchanjaji, ubora na watoa huduma pale inapohitajika.

Yaliyomo

Mimea yenye afya	2
Chakula na virutubisho muhimu	6



Mazingira salama kwa ustawi wa jamii	8
Ushauri kwa wafugaji wa kuku	12

Mpendwa Mkulima

Ndugu msomaji wa Jarida la Mkulima Mbunifu, heri yam waka mpya 2025. Ni matumaini yetu kuwa mwaka umeanza vyema, na hatuna budi kumshukuru Mungu

Ikiwa ni toleo letu la kwanza kwa mwaka huu 2025, ni imani yetu kuwa malengo na mikakati uliyoiweka umeanza kutekeleza kwa kwani huu ni msimu wa kupanda.

Hakikisha pia unapata elimu sahihi itakayokusaidia katika shughuli zote za kilimo, ufugaji na usindikaji ili uweze kufanya kwa mafanikio na kwa tija zaidi.

Kama ni kwenye kilimo, hakikisha ufahamu kuhusu mbegu bora na upatikanaji wake, namna ya kupanda, matunzo, namna ya kukabiliana na wadudu na magonjwa, namna ya kuvuna na kuhifadhi, lakini kubwa zaidi namna ya kupata na kufikia soko.

Vilevile kwa upande wa mifugo, hakikisha unafahamu unataka kufuga nini, mbegu bora, utunzaji, namna ya kudhibiti magonjwa, lishe, mpaka namna ya kufikia soko la bidhaa za mifugo yako.

Usisahau, Mkulima Mbunifu ni moja ya vyanzo vya kuaminika na kuwa na uwezo mkubwa wa kukusaidia kwa maarifa ya kilimo, ufugaji na usindikaji. Zingatia yale yanayochapishwa katika jarida hili na machapisho mengineyo ya MkM na hakika utaona mafanikio yake.

Mwisho, Mkulima Mbunifu itakufikia kwa njia ya simu kufanya tathmini ya jarida hili kwako, hivyo tunaomba ushirikiano. Vilevile unaweza kuwasiliana nasi kwa maswali, maoni na mrejesho juu ya mafanikio ya kusoma jarida hili.

Zingatia afya ya mimea ili kupata mapato mengi

Mara nyingi wakulima wanapuuzwa maswala yanayohusiana na nafya ya mimea na kupata hasara kubwa. Ikiwa mkulima hatawekeza muda na rasilimali, atakuwa na mimea iliyodhoofika.

Juma Mchinja

Ni nia ya kila mkulima kuwa na mimea yenye nguvu na afya, na yenye uwezo wa kutoa mapato ya hali ya juu. Ni lazima kuwa makini na kuzingatia mbinu zitakazowezesha kufikia lengo hili. Hivyo, swala zima la afya ya mimea huanzia kwenye utayarishaji wa shamba, kurutubisha udongo, kuchagua mbegu na kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa.

Haya ni baadhi ya mambo ya kuzingatia ili kuweka mimea kwenye hali ya afya na kuzalisha zaidi.

Tunza udongo ili kutunza mimea

Utunzaji wa udongo unategemeana kwa kiasi kikubwa na mazingira ya kibiolojia. Kazi kubwa ya baadhi ya viumbe hai waliomo kwenye udongo, ni kumeng'anya mabaki ya mimea na viumbe hai wengine. Mtiririko huu hufanya uwepo wa nguvu, virutubisho, na hewa ya kaboni, ambavyo kwa pamoja hutengeneza rutuba kwenye udongo.

Utunzaji wa rutuba ya udongo unaongozwa na filosofia hii 'Lisha udongo ili nao ulishe mimea.' Udongo wenye rutuba utazalisha mimea yenye afya inayoweza kukabiliana na magonjwa.

Uzalishaji wa mazao kwa njia za asili uhakikisha kunakuwepo uzalishaji wa kutosha bila ya kutumia pembejeo za ziada isipokuwa matandazo, mboji na bila kutifua udongo mara kwa mara. Ongezeko la malighafi za asili husaidia kuimarisha udongo na kufanya kuwepo kwa virutubisho vya kutosha.

Aina ya kilimo cha kisasa na kinachotumia kemikali hufanywa tofauti na ilivyo kwa kilimo hai.



Picha:IN

Katika aina hii ya kilimo; udongo hulimwa mara kwa mara jambo linalosababisha uharibifu wa muundo wa udongo, uwiano wa virutubisho, ambapo virutubisho huongezwa kwa kutumia mbolea za viwandani na matandazo hayazingatiwi.

Muundowa udongo unapobadilika, rutuba nayo hupungua, uwezo wa udongo kuhifadhi maji pamoja na viumbe hai kwenye udongo pia hupungua.

Kiwango cha udongo mzuri pia hupungua kwa kuwa hakuna tena

viumbe hai wanaotengeneza udongo pia inapungua mazao kila msimu. Kwa asili mzunguko huu huwa na matokeo yanayoishia kwenye afya ya mimea, na hapa wadudu huchukua nafasi inayowawezesha kufikia malengo yao.

Usafi shambani

Ni vyema kuhakikisha kwamba shamba ni safi, haina magugu ambayo yanaweza kushindana na mimea kupata lishe na maji. Inashauriwa kufanya palizi ya mara kwa mara. Pia, Panda mimea ya msimu ikifuatana na

mimea ya msimu mfupi. Kwa, mfano, baada ya kupanda mahindi, unaweza kupanda viazi vitamu ambavyo vitasaidia kufunika udongo na kuhakisha upotevu mdogo wa maji.

Tumia wadudu rafiki dhidi ya wadudu waharibifu

Kuna baadi ya mimea kama vile nyanya ambayo wakulima wamekuwa wakitegemea sana kwa ajili ya kujipatia kipato wakati wakisubiria mazao yanayochukua muda mrefu kama vile, mahindi na mengineyo. Kwa bahati mbaya nyanya ni moja ya mazao ambayo ni rahisi sana kushambuliwa na wadudu katika mzunguko wake wa uzalishaji.

Mbali na nyanya mazao mengine ambayo ni rahisi kushambuliwa ni viazi mviringo, maharagwe, sukuma wiki, hoho, spinachi na kabichi. Madhara zaidi hutokea kunapokuwepo na upungufu mkubwa wa wadudu rafiki. Mkulima anapotumia kemikali kuulia wadudu, sumu hizo haziui wadudu waharibifu tu ila pia huuwa na wadudu rafiki ambao hutumika kudhibiti wadudu waharibifu kwa njia ya asili. Hii ndiyo sababu wadudu waharibifu wamekuwa wengi mashambani.

Tumia dawa za asili

Mojawapo ya wadudu ambao huwa wakulima hupata shida kuwadhhibiti, ni inzi weupe, vithiripi, buibui wekundu, na vidukari. Wadudu hawa huharibu kati ya asilimia 20-30 ya mazao na kuendelea. Wadudu kama vithiripi na inzi weupe ni vigumu sana kuwadhhibiti kwa kuwa huzaliana kwenye mazao yanayokua. Hivyo, njia moja wapo ni kutumia njia ya kujihami badala ya wakulima kutumia kemikali, wanaweza kutumia dawa za asili ambazo haziui wadudu rafiki na ambazo pia husaidia mimea



Picha:MKW

kujijengea kinga dhidi ya magonjwa.

Punguza matumizi ya kemikali

Wakulima wengi hutumia dawa za kemikali kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu shambani. Hata hivyo, tatizo moja kubwa la kutumia dawa za kudhibiti wadudu na magonjwa kwa kiasi kikubwa ni kuwa wadudu hao huwa sugu baada ya muda mfupi.

Hii inapelekea wakulima wengine kubuni njia hatari za kudhibiti wadudu na magonjwa. Baadhi yao hutumia dawa ya kuulia kupe kwa ajili ya kuuwa wadudu kama vile inzi weupe, vithiripi, utitiri na buibui. Hii ni hatari sana kwani dawa hii inaruhusiwa kutumika kwa ajili ya kuogeshea wanyama tu lakini si kwenye mboga ambazo zinauzwa kwa walaji. Hali hii inahatarisha afya ya walaji.

Pia, kuna aina nyingine za dawa ambazo ni hatari na zimepigwa marufuku na serikali, lakini maduka mengine ya pembejeo bado yanaziua na wakulima wanatumia. Aina hizi za kemikali ni hatari sana kwa afya

ya binadamu hasa zinapojikusanya kwa kiasi kikubwa mwilini. Baada ya muda mrefu inaweza kuwa sugu na kusababisha magonjwa kama saratani, ukuaji usiokuwa wa kawaida, kisukari na magonjwa ya mzio.

Mbali na madhara kwa afya ya binadamu, pia sumu hizo hupenya na kwenda kwenye maji yaliyomo ardhini na kuyachafua. Sumu hizo huathiri na kuuwa wadudu muhimu waliomo ardhini ambao huboresha udongo, kuuwa wadudu muhimu ambao hufanya ushavushaji kwenye mazao, na wadudu wengineo ambao hudhibiti wadudu waharibifu kwenye mazao na mazingira yetu. Hivyo, inashauriwa wakulima kutumia mbinu endelevu za kudhibiti wadudu na magonjwa.

Uchunguzi wa mara mara

Ni vyema mkulima kutembelea shamba lake mara kwa mara na kuangalia hali ya mimea yake. Hii inasaidia kutambua kama mimea imepata maambukizi ya magonjwa na kujua vile atapambana na hali hiyo. Huenda vijidudu vimeanza kuvamia mimea ili hali mkulima hajatambua. Ikiwa mkulima atatembelea na kutazama mimea yake, basi huenda akaepukana na magonjwa na pia kuhakikisha kwamba anazuia na kutibu mimea yake kwa wakati unaofaa.

Kawaida huwa tunashauri mkulima kuwa na uhusiano na afisa wa kilimo kata. Afisa anaweza kutoa ushauri kuhusu usimamizi mzuri wa mimea na pia mipango thabiti ili kuhakikisha uzalishaji wa hali ya juu.



Picha:IN

Mkulima Mbunifu ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika Nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni mojawapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linafadhiliwa na Biovision Foundation



Wachapishaji: African Insect Science for Food and Health (ICIPE), S.L.P 30772 – 00100 Nairobi, Kenya, Simu: +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org

Mpangilio: Cathbert Msemo 0757 847 481

Mhariri: Erica Rugabandana

Mhariri Msaidizi: Flora Laanyuni

Anuani: *Mkulima Mbunifu*

Sakina, Majengo road, (Elerai Construction Block)

S.L.P 14402, Arusha, Tanzania

Ujumbe mfupi pekee: 0785 496 036, 0766 841 366

Piga simu: 0717 266 007, 0762 333 876

Barua pepe: info@mkulimambunifu.org

www.mkulimambunifu.org

Je, Unaelewa vema juu ya afya ya Mifugo? Tujikumbushe

Kawaida, ufugaji una madhumuni ya uzalishaji wa bidhaa tofauti. Inajumhisha hali yao ya kimwili, kiakili na kihisia. Kwa wakulima wadogo, kuhakikisha afya ya mifugo kama vile ng'ombe, nguruwe, kuku na mbuzi ni muhimu sio tu kwa uendelevu wa kiuchumi lakini pia kwa usalama wa chakula na maisha ya familia nyingi.

Eliudi Letungaa

Afya ya mifugo hujumuisha hali kamili ya wanyama wa shambani. Yaani, uwezo wao wa kukua, kuzalisha na kuleta faida kwa mkulima. Hii ni pamoja na lishe na uangalizi bora, ukosefu wa ugonjwa, afya ya uzazi, na kuwa na maisha marefu. Mifugo yenye afya bora huzaa zaidi, hutoa nyama bora, maziwa na mayai, ambayo ni muhimu kwa matumizi ya ndani na soko.

Katika mikoa ambayo wakulima wadogo wanategemea sana mifugo kwa ajili ya maisha yao, kuelewa na kuweka kipaumbele afya ya mifugo inakuwa muhimu sana. Ikiwa afya ya mifugo itazorota, basi atapata hasara, na kupoteza muda na rasilimali.

Umuhimu wa afya ya mifugo una mambo mengi. Kiuchumi, wanyama wenye afya nzuri huchangia uzalishaji wa juu na kupunguza gharama zinazohusiana na udhibiti wa magonjwa na matibabu ya mifugo. Kwa wakulima wadogo katika maeneo



Picha:IN

mengi nchini, ambapo rasilimali zinaweza kuwa chache, mifugo yenye afya inaweza kumaanisha tofauti kati ya maisha mazuri yenye uwezo wa kukidhi mahitaji na umaskini.

Aidha, afya ya mifugo ina mchango mkubwa katika usalama wa chakula. Kwa kuongezeka kwa idadi ya watu, mahitaji ya nyama, maziwa, na bidhaa za kuku yanaongezeka. Kuhakikisha kwamba mifugo ina afya bora huongeza ubora na wingi wa chakula kinachopatikana kwa jamii. Zaidi ya hayo, mifugo yenye afya nzuri husaidia kuzuia mlipuko wa magonjwa yanayoweza kupitishwa kutoka kwa

mifugo hadi kwa wanadamu, hivyo kulinda afya ya mifugo ni kulinda usalama wa umma.

Kanuni za afya ya mifugo

Lishe

Lishe bora ni msingi wa afya ya mifugo. Mifugo huhitaji lishe bora yenye virutubisho muhimu kwa ukuaji, uzazi na kinga na uzalishaji. Wakulima wanapaswa kuzingatia kutoa malisho, nafaka, na virutubisho vinavyofaa kwa kila aina ya mifugo, iwe ng'ombe, nguruwe, kuku na mbuzi, na kadhalika. Hii ni kulingana na umri wao, hali ya afya, na mahitaji ya uzalishaji.

Kwa mfano, kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, maziwa ya kwanza ya ng'ombe yanajenga kinga mwili wa ndama dhidi ya magonjwa, na yana virutubisho vya proteni vinavyochochea ukuaji wa haraka. Hivyo, ndama anaponyimwa maziwa ya kwanza (*colostrum*) uwezo wake wa kukua unaadhirika, anadumaa na baadaye akiwa ng'ombe mkubwa, uwezo wake wa uzalishaji wa maziwa unakuwa wa chini mno.

Kwa wafugaji wa kuku, chakula chenye virutubisho vya protein, wanga, na madini na vitamin kwa viwango vinavyofaa ni muhimu kwa uzalishaji wa mayai mengi. Usipowalisha kuku vizuri, watakunyima mayai!

Usafi na usalama wa mazingara

Utekelezaji wa kanuni bora za usafi na hatua za usalama wa viumbe



Picha:IN

ni muhimu katika kuzuia kuanza na kuenea kwa magonjwa. Hii ni pamoja na kusafisha mara kwa mara mabanda/makaazi ya mifugo, kuhakikisha upatikanaji wa maji safi kwa matumizi ya mifugo, na kuwatenga wanyama wagonjwa ili kupunguza hatari ya kuambukizana.

Wakulima wanaweza kufuata mazoea rahisi kulingana na upatikanaji wa nguvu kazi, lakini yanayoleta usalama wa mifugo, mfano, kudhibiti watu wanaoingia shambani au mabanda ya mifugo kwa kuweka maji ya dawa. Hii ni pamoja na magari na vifaa vinavotumika bandani au vifaa vinavyotoka kwa wafugaji wengine, ili kuepukana na magonjwa yanayotoka nje.

Pamoja na hayo, mazingara ambayo mifugo hufugwa huathiri sana afya yao. Jenga banda/nyumba inayofaa ambayo hutoa nafasi ya kutosha, kuingiza hewa safi, na ulinzi wa kutosha kwa mifugo. Kwa mfano,

kuku wanaofugwa katika mazingira ya msongamano mkubwa wanaweza kupata msongo wa mawazo na kushambuliwa zaidi na magonjwa. Mkulima anapaswa kujitahidi kutoa hali zinazokuza faraja kwa mifugo.

Uchunguzi wa mara kwa mara

Kwa kawaida, mfugaji anashauriwa kushirikiana na afisa wa mifugo ugani aliye karibu. Afisa huyu anaweza kutoa huduma ya mara kwa mara ili kujua wakati mifugo wanaaza kuwa wagonjwa ili kutoa tiba ya haraka na kushauri mbinu za kuzuia mkurupuko wa magonjwa. Hii ni pamoja na chanjo, dawa za minyoo na ufuatiliaji wa afya kwa ujumla.

Anzisha leo, uhusiano na daktari wa mifugo wa ndani ili kuhakikisha kwamba mifugo wako wanapata matibabu ya haraka inapohitajika. Kupima afya mara kwa mara sio tu husaidia kutambua magonjwa mapema lakini pia huchangia

uzalishaji bora. Pia, anaweza kushauri taratibu za ulishaji.

Faraja na ustawi wa akili

Afya ya mifugo sio mahitaji ya kimwili pekee, bali pia ustawi wa akili na kukaa kwa amani na furaha. Mambo ya kushughulikia kwa mkazo ni pamoja na kuepuka kuishi kwa hali duni na kutengwa kwa mifugo ambapo unawakosesha kutangamana. Mkulima anapaswa kuwashughulikia mifugo kwa upole, kuwapa nafasi ya kutosha ya kutangamana na kuboresha mazingira yao ili kukuza tabia asili za mifugo.


Masuala ya kawaida

Mifugo huwa wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiafya zinazoweza kuathiri uzalishaji wao. Kwa mfano, ng'ombe huwa na magonjwa kama vile ugonjwa wa kiwele na matiti, magonjwa yanaoletwa na kupe, na pia upungufu wa lishe. Nguruwe wanaweza kupata matatizo kama vile homa ya nguruwe, wakati kuku wanaweza kuathiriwa na magonjwa kama vile kideri, homa na magonjwa mengine ya kupumua. Hivyo, mfugaji anapaswa kuwa macho na kutekeleza hatua za kinga kama vile chanjo na mbinu bora za usimamizi ili kupunguza hatari hizi.

Kuweka kipaumbele afya ya mifugo ni juhudi za kimsingi kwa wafugaji na inachangia uzalishaji wa hali ya juu, kuboresha mapato ya wafugaji, na usalama wa chakula na afya ya jamii kwa ujumla. Kwa kuzingatia lishe bora, usafi, uchunguzi wa mara kwa mara, wafugaji wanaweza kuhakikisha uendelevu na tija ya mifugo yao.



Picha:IN



Picha:IN

Chakula na virutubisho muhimu katika mwili wa binadamu

Chakula ni muhimu kwa binadamu wote kwani huupatia mwili virutubishi mbalimbali kwa ajili ya kazi mbalimbali mwilini na hivyo kuwezesha kuwa na afya bora. Karibu vyakula vyote huwa na virutubishi zaidi ya kimoja ila hutofautiana kwa kiasi na ubora. Kila kirutubishi kina kazi yake muhimu mwilini na mara nyingi virutubishi hutegemeana ili viweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Nchini Tanzania kuna matatizo mengi ya utapiamlo ambayo yanatokana na kuzidi au kupungua kwa virutubishi. Tatizo la kuzidi kwa virutubishi ambalo linakua katika baadhi ya jamii linahusishwa kwa karibu na magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza. Utapiamlo uwe wa kupungua au kuzidi kwa virutubishi huleta athari kwa jamii ikiwa ni pamoja na zile za kibinafsi, kijamii na kiuchumi.

Aina za virutubishi

Kuna aina kuu tano za virutubishi ambavyo ni kabohaidreti, protini, mafuta, vitamini na madini. Kila kirutubishi kina kazi yake katika mwili wa binadamu na kiasi kinachohitajika hutofautiana.

Jedwali linalofuata linaonesha baadhi ya virutubishi pamoja na umuhimu wake, vyanzo vyake na dalili zinazojitokeza upungufu unapotokea.

Eliudi Letungaa

	Aina	Umuhimu	Vyanzo	Dalili za upungufu
1	Kabohaidreti	Kuupa mwili nishati lishe/nguvu kwa ajili ya kufanya kazi mbalimbali pamoja na kuupa joto. Kabohaidreti ndiyo inayochukua sehemu kubwa ya mlo. Kabohaidreti inajumuisha sukari, wanga na makapi-mlo.	Mahindi, mchele, ngano, uwele, mtama, ulezi, aina zote za viazi, muhogo, magimbi, ndizi, asali, sukari, baadhi ya matunda	Mwili kukosa nguvu na kupungua uzito Utapiamlo wa upungufu wa nishati-lishe na protini
2	Protini	Ukuaji wa mwili na akili kutengeneza seli mpya za mwili, kukarabati seli zilizochokaa au kuharibika; kutengeneza vimeng'enyoy, vichocheo, damu na mfumo wa kinga, huupa mwili nguvu pale ambapo kabohaidreti haitoshelezi mahitaji ya mwili.	Aina zote za nyama, vyakula vya jamii ya kunde (maharagwe, kunde, njegere, mbaazi, choroko, dengu, njugu, n.k), karanga korosho, samaki, dagaa, wadudu (kama senene na kumbikumbi), maziwa, jibini, mayai	Ukuaji duni na maendeleo hafifu kwa watoto, Utapiamlo wa upungufu wa nishati-lishe na protini
3	Mafuta	Kuupa mwili nguvu, joto na kusaidia ufyonzaji wa baadhi ya virutubishi kama vitamini A, D, E na K. Mafuta pia hulainisha chakula na kukifanya kiwe na ladha nzuri, na hivyo kumfanya mlaji ale chakula cha kutosha.	Siagi, samli, karanga, samaki wenye mafuta, jibini, nyama iliyonona (nundu, nyama ya nguruwe, mkia wa kondoo), nazi, kweme, mawese, mbegu zitoazo mafuta kama alizeti, ufuta, maboga, korosho, mawese, na pamba na mafuta yaliyotengenezwa maalum kwa kupikia.	Mwili kukosa nguvu na kuwa dhaifu, ngozi kuwa ngumu na yenye magamba, dalili za upungufu wa vitamini A, D, E na K
4	VITAMINI: Vitamini zinahitajika mwilini kwa ajili ya kuulinda mwili dhidi ya maradhi pamoja na kuufanya mwili ufanye kazi zake vizuri. Kuna aina nyingi za vitamini na zinapatikana kwa wingi kwenye mboga-mboga, matunda, dagaa na samaki pia kwenye vyakula vinavyotokana na wanyama kama maziwa, aina zote za nyama, na mayai. Pia vitamini nyingine hupatikana kwenye nafaka mfano kundi la vitamini B. Zifuatazo ni baadhi ya aina za vitamin:			
I.	Vitamini A	Ukuaji wa akili na mwili, kuimarisha seli za ngozi, kuimarisha kinga ya mwili dhidi ya maradhi, kusaidia macho kuona vizuri kulinda utando laini katika sehemu mbalimbali za mwili.	Maini, figo, mayai, samaki, nyama jibini, siagi mboga za majani zenye rangi ya kijani, viazi vitamu vya njano, maboga, karoti, nyanya, mawese na matunda hasa yenye rangi ya njano au nyekundu kama papai, embe, n.k.	Kutoona kwenye mwanga hafifu, kovu kwenye jicho, maradhi ya kuambukiza ya mara kwa mara hasa katika mfumo wa hewa, ngozi kukosa unyororo
II.	Kundi la Vitamini B <i>B1 Thiamin B2 Riboflavin B3 Niacin B5 Biotin B6 Pyridoxine B9 Folic Acid Cynocaobal-amin</i>	Kusaidia mwili kufanya kazi sawa sawa hasa katika mfumo wa chakula, kinga na fahamu. Huwezesha moyo na misuli kufanya kazi kwa ufanisi. Husaidia kutengeneza seli mpya na kukarabati seli za neva na seli nyekundu za damu.	Maini, viazi, maziwa, nafaka zisizokobolewa, vyakula vya jamii ya kunde, uyoga, karanga, mayai, kuku, samaki, nyama, matikiti, parachichi, ndizi mbivu, chungwa, mboga za majani za kijani, mbegu za alizeti na za maboga, korosho na vyakula vilivyochachushwa kama mtindi na togwa.	Kunyongea na kusikia uchovu, Kukosa hamu ya kula kupungua uzito, maumivu mwilini, moyo na mfumo wa chakula na wa fahamu kushindwa kufanya kazi vizuri, vidonda kwenye kona za midomo, kuhara, magonjwa ya ngozi, kuchanganyikiwa, kukosa usingizi, kuumwa kichwa na upungufu wa damu

III.	Vitamini C	Kusaidia matumizi ya madini ya chokaa, ufyonzaji wa madini chuma, huboresha kinga ya mwili na kuondoa chembe haribifu mwilini. Husaidia kuimarisha mishipa ya damu, huzuia uvujaji wa damu ovyo, husaidia umetaboli wa protini.	Mapera, machungwa, nyanya, ukwaju, malimau, ndimu, machenza, madalansi, ubuyu, pesheni, mabungo, na aina nyingine za matunda pori na mboga za majani.	Kutoka damu kwenye fizi na ngozi, kuvimba kwa viungio, vidonda kutopona haraka, kuoza meno, mishipa ya damu kupasuka kwa urahisi, upungufu wa damu
IV.	Vitamini E	Huondoa chembe haribifu mwilini, husaidia umetaboli wa seli za damu, huimarisha kinga ya mwili, hupunguza kasi ya seli kuzeeka kiurahisi, hukinga seli nyekundu za damu kuharibiwa na chembe haribifu mwilini; kinga dhidi ya saratani.	Mboga za majani zenye rangi ya kijani, mbegu zitoazo mafuta, maini, mayai, siagi, nafaka zisizokobolewa, karanga na korosho	Upungufu hutokea kwa nadra pale ambapo kuna tatizo la ufyonzaji wa mafuta mwilini. Misuli ya moyo na neva kuharibika.
5	MADINI: Madini kama zilivyo vitamini huulinda mwili dhidi ya maradhi na kuufanya ufanye kazi zake vizuri. Kuna aina nyingi za madini. Baadhi ya vyakula vyenye madini kwa wingi ni pamoja na vyakula vinavyotokana na wanyama, dagaa, samaki, mboga-mboga na matunda. Zifuatazo ni baadhi ya aina za madini:			
I.	Madini chuma	Kutengeneza seli nyekundu za damu, kusafirisha hewa ya oksijeni kwenye damu, kusaidia utumikaji wa nishati-lishe, kudhibiti chembe haribifu mwilini	Maini, figo, bandama, nyama nyekundu, samaki, dagaa, kuku, mboga za majani zenye rangi ya kijani, vyakula vyaa jamii ya kunde, baadhi ya matunda yaliyokaushwa, rozela/ choya na baadhi ya nafaka	Upungufu wa damu, ngozi na sehemu nyeupe ya macho kuwa nyeupe kuliko kawaida, mwili kukosa nguvu, kukosa usingizi, kupumua kwa shida, moyo kwenda mbio
II.	Madini ya Chokaa	Kujenga na kuimarisha mifupa na meno, kusaidia damu kuganda baada ya kuumia, kusaidia misuli na moyo kufanya kazi vizuri, huboresha kinga ya mwili, huboresha mfumo wa fahamu, husaidia figo kufanya kazi vizuri	Maziwa na bidhaa zake, mboga za majani zenye rangi ya kijani, samaki wakavu, maharagwe, ulezi, mtama, dagaa, bamia, mbegu zitoazo mafuta, karanga na korosho	Mifupa na meno kuwa laini na kuvunjika kwa urahisi, matege kwa watoto, ukuaji hafifu kwa watoto
III.	Zinki	Kuboresha kinga ya mwili, kusaidia uyeyushwaji wa chakula na usafirishwaji wa Vitamini A mwilini, kuzuia chembe haribifu, husaidia kutengeneza protini mwilini na kupona kwa vidonda, husaidia katika ukuaji na maendeleo ya mfumo wa uzazi.	Nyama, kuku, samaki, jibini, maziwa, nafaka zisizokobolewa, vyakula vya jamii ya kunde na mboga-mboga, uyoga, vitunguu maji, mayai, maini, mbegu za maboga, pilipili manga, karanga na korosho.	Kuchelewa kwa wavulana kubalehe na wasichana kupata hedhi, vidonda kuchelewa kupona, mapele kwenye ngozi, kuharisha, ukuaji hafifu wa watoto, ugumba, kutokuwa makini, vidonda vya ngozi, kupungua hamu ya kula
IV.	Madini joto	Ukuaji na kusaidia ubongo na mfumo wa fahamu kufanya kazi vizuri	Vyakula vya baharini, chumvi iliyowekwa madini joto, vyakula vyote vilivyozalishwa kwenye udongo wenye madini joto	Kuvimba tezi la shingo, uwezo mdogo wa ubongo wa kufanya kazi, uelewa mdogo katika masomo, kuzorota na mwili kukosa msukumo wa kufanya shughuli yeyote, kudumaa mwili

JINSI YA KUKADIRIA KIASI CHA MLO KWA KUTUMIA MIKONO YAKO

Mikono yako inaweza kutumika kukadiria kiasi cha chakula unachotakiwa kula kwa mlo mmoja. Ufuatao ni muongozo wa kukadiria kiasi cha mlo kwa kutumia mikono kama kipimo:

1. Vyakula vya nafaka, mizizi na ndizi kama vile ugali, wali, viazi:



Kiasi sawa na ukubwa wa ngumi moja



2. Matunda

Kiasi cha matunda ni sawa na ngumi moja; mfano saizi ya kati ya chungwa, embe, kipande cha papai, tikiti-maji, au nanasi.

3. Mboga-mboga:



Kiasi cha mboga mboga kiwe kingi zaidi, kadiri kiasi cha kuweza kujaa katika viganja vya mikono yote miwili.

4. Vyakula vya jamii ya kunde na vile vyenye asili ya wanyama:



Kiasi sawa na ukubwa wa giganja cha mkono wako na unene uwe sawa na wa kidole kidogo cha mkono wako.

5. Mafuta:

Ncha ya kidole gumba.



Mazingira salama ni nguzo ya mafanikio kwa ustawi wa jamii

Je, umewahi kusikia kuhusu mazingira salama na yenye afya? Lakini je, umewahi kujiuliza mazingira salama yakoje!

Magrathe Mollel

Kwa ufupi, mazingira yenye afya na salama ni muhimu kwa ustawi wa jamii yoyote ile kwa sababu yanatoa fursa ya hewa safi, maji salama, ardhi yenye rutuba, na kuhakikisha muingiliano chanya baina ya jamii na mazingira husika. Hata hivyo, kuna changamoto mbalimbali zinazochangia uharibifu wa mazingira na kupelekea kutishia usalama wake. Changamoto hizo ni kama vile utupaji holela wa plastiki, uchomaji wa taka unaosababisha usambaaji wa hewa ukaa, matumizi ya viuatilifu kupita kiasi, na usimamizi duni wa taka.

Makala hii itaelezea kwa kina mazingira salama, madhara ya uharibifu wa mazingira, na mchango wa jamii kwenye utunzaji wa mazingira. Pia, itaangazia afya ya mazingira kwenye kilimo ikolojia na kutoa maoni ya nini kifanyike ili kuhakikisha usalama wa mazingira.

Nini maana ya mazingira salama?

Mazingira salama ni mazingira yanayokidhi afya ya binadamu na bioanuwai. Ni mazingira yenye hewa safi, vyanzo vya maji visivyo na uchafu, na udongo wenye rutuba. Kwa maana

nyingine mazingira salama ni yale yenye uchafuzi mdogo na usio na madhara kwenye afya ya binadamu wala mifumo ikolojia.

Faida ya mazingira salama


Faida za mazingira salama na yenye afya ni pamoja na upatikanaji wa hewa safi ambayo hupunguza magonjwa ya kupumua, na maji safi ambayo hupunguza magojwa yatokanayo na maji machafu. Pili, husaidia uzalishwaji wa chakula safi, salama na bora na pia huongeza tija kwenye uchumi kupitia biashara za kilimo hai.

Athari za uharibifu wa mazingira

Uharibifu wa mazingira husababishwa na shughuli za kibinadamu pamoja na mitazamo hasi juu ya mazingira, mfano utupaji holela hasa taka ngumu kama plastiki, matumizi ya kemikali hatari kupita kiasi, uchomaji wa taka na kukata miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali mfano kilimo.

Uchafuzi wa plastiki

Uchafuzi wa plastiki ni moja kati ya matishio makubwa kwenye afya ya jamii na usalama wa mazingira.



Picha:IN

Plastiki zinatumiwa katika maeneo mengi na mara nyingi baada ya matumizi yake huishia kutupwa kama takataka na kuzagaa mitaani. Katika hali tofauti plastiki hizi huenda kuziba njia za maji, na kudhuru wanyamapori, samaki na viumbe wengine.

Kwa upande mwingine, plastiki hizi huweza kuwa na kemikali hatari kwa maji na udongo. Vile vile, kuna jamii ambazo huchoma plastiki kwa sababu mbalimbali ikiwemo, kukosa matumizi au kutokuwa na mahali maalum pa kuzitupa. Moshi unaotokana na kuchoma huko huweza kuwa na sumu zinazoweza kusababisha matatizo ya kupumua na masuala mengine ya kiafya kwa jamii.

Matumizi ya viuatilifu kupita kiasi

Dawa za kuuwa wadudu hutumiwa sana kulinda mazao, lakini matumizi kupita kiasi yanaweza kuwa na matokeo mabaya. Mabaki yanaweza kuchafua vyanzo vya maji, kudhuru aina mbalimbali za viumbe visivyolengwa kama vile nyuki, na kuhatarisha afya ya binadamu. Kwa mfano, kutiririka kwa dawa kwenye mito kunaweza kuuwa samaki na viumbe vingine vya majini, na hivyo kuvuruga mzunguko wa chakula na maisha yanayotegemea uvuvi.

Mazingira salama katika kilimo ikolojia

Mazingira yenye afya na salama ndio msingi wa mafanikio ya kilimo cha ikolojia. Hii ni kwa sababu mazingira haya ndiyo msingi wa bioanuwai, rutuba ya udongo, uhifadhi wa maji, na uthabiti wa jumla wa mfumo ikolojia. Kudumisha mazingira yenye

afya na salama ni hitaji la kila mkulima katika kufikia mifumo endelevu na yenye tija ya kilimo.

Mazingira haya yanajumuisha bioanuwai mbalimbali kuanzia viumbe vidogo vilivyo udongoni hadi mimea, wadudu na wanyama wakubwa zaidi. Udongo imara wenye viumbe hai, vijidudu, na ukiwa na muundo mzuri huhakikisha upatikanaji wa virutubisho, uhifadhi wa maji, na ustahimilivu dhidi ya mmomonyoko. Vyanzo safi vya maji kwa ajili ya umwagiliaji, mifugo na mazao bora. Pia, mazingira haya yanazingatia matumizi madogo sana ya kemikali hasa pale inapolazimu pamoja na udhibiti sahihi wa taka.

Kwa nini mazingira salama ni muhimu kwa mkulima

Husaidia kuimarisha uzalishaji kwa kuwa udongo wenye afya na salama hupunguza utegemezi wa mbolea za kemikali na kuboresha kiwango na ubora wa mazao.

1. Hupunguza gharama kwani mkulima huepukana na utegemezi wa pembejeo na kemikali kwa kutumia huduma za asili.
2. Huoresha ustahimilivu wa mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mbinu kama vile kilimo mseto na mseto wa mazao ambavyo husaidia kupunguza athari za hali mbaya ya hewa.
3. Hudumisha usalama wa mifumo ikolojia na kuhakikisha kwamba ardhi inaendelea kuwa na tija na yenye manufaa kwa vizazi vijavyo vya wakulima.
4. Huongeza fursa za masoko hasa



Picha:IN

Uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji

kwa wateja wanaopendelea bidhaa zinazokuzwa kwa njia za asili ambao idadi yao inazidi kuongeza siku hadi siku.

Nafasi ya jamii katika kuhakikisha mazingira salama

1. Kupeana ujuzi na uzoefu hususani ufahamu kuhusu mbinu za kilimo-hai, kupunguza taka hatari, na hatari za uchafuzi wa mazingira.
2. Kupanda na kuhifadhi miti, na kulinda misitu ya jamii.
3. Kutumia njia za asili mfano, kutengeneza na kutumia mbolea ya mboji, kuvuna na kutumia maji ya mvua, pamoja na matumizi ya nishati mbadala.
4. Kushirikiana katika kufanya usafi wa mazingira hasa kukusanya taka za plastiki na nyinginezo.
5. Kufata kanuni na sheria ndogo

zilizowekwa na kufanya kazi kwa ukaribu na serikali za mitaa ili kuhakikisha usalama wa mazingira.

Hatua gani zimefanyika?

Kwanza kabisa kuna baadhi ya jamii ambazo zimetambua madhara ya uchafuzi wa plastiki na wameanza kushirikiana kupunguza matumizi ya plastiki, na pia kubadilisha plastiki ambazo zingetumika mara moja na kuzitumia tena. Mfano, kutumia mifuko, na chupa zaidi ya mara moja.

Pia, baadhi ya wanajamii wameweza kutumia rasilimali zao kikamilifu kuzalisha mazao na kutunza bioanuwai. Mfano, kutundika mizinga kwenye miti iliyopo katika mashamba yao, njia ambayo imekuwa na tija kwani wameweza kutumia njia asilia kudhibiti wadudu, wakati mizinga hiyo ikisaidia kuchavusha mazao ya karibu kupitia nyuki wake.


Shule zimekuwa mstari wa mbele kuelimisha watoto kuhusu hatari ya taka za plastiki. Wakati huo huo serikali imejitahidi kuondoa mifuko ya plastiki na kuwapa wafanyabiashara njia mbadala hasa kutumia vifungashio vinavyoweza kuharibika bila kuathiri udongo.

Hitimsho

Pamoja na hayo yote bado kuna jukumu kubwa kwa kila mwanajamii kuwa mstari wa mbele kuhakikisha usalama wa mazingira katika nyanja zote. Pia, serikali kuendeleza jitihada na mipango kabambe ya kusimamia sheria endelevu kwa ajili ya mazingira salama.



Picha:IN



Picha:IN

Jarida la MkM limetupa hamasa ya kutekeleza shughuli zetu za uzalishaji

Kuna msemu aliowahi kuutoa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuwa; "Elimu sio njia ya kuepuka umasikini bali ni njia ya kupigana na umasikini". Msemu huu wameudhirisha wazi na kwa vitendo wakulima wajasiriamali wa kikundi cha kusindika kitarasa a-mbao wametumia elimu inayotolewa na jarida la Mkulima Mbunifu kupiga vita umaskini na kufanikiwa.

Flora Laanyuni

Kikundi hiki kinachofanya shughuli mbalimbali za uzalishaji kama vile kilimo ikolojia, usindikaji hasa wa unga wa kitarasa, unga wa mbegu za maboga, pamoja na mafuta ya parachichi wameonyesha hamasa kubwa na kujivunia jarida la *Mkulima Mbunifu*.

"Huu ni mwaka wa tatu sasa toka tumeanza kupokea jarida la *Mkulima Mbunifu*, na kwa hakika tumefaidika kwa mengi kupitia elimu inayotolewa huko na kila mkulima ana kitu cha kukumbuka kupitia jarida hili". Alisema mwenyekiti wa kikundi hiki Bw. Antipas Shao.

Wakulima hawa wanasema kuwa, kupitia kusoma jarida la *Mkulima Mbunifu*, kila siku wanapata hamasa ya kuendelea kufanya shughuli za kilimo, ufugaji na ujasiriamali kwani pale wanaposoma na kujionea jinsi wengine walivyofanya na kufanikiwa, hakika wanapata moyo na kuzidi kufanya kazi zao kwa nguvu na kwa

umoja.

Angelina Kimaro (M/Hazina wa kikundi) anasema kuwa, "jarida hili limekuwa chachu kwetu kwani linatufundisha mambo mengi yahasuyo kilimo na ufugaji pamoja na ujasiriamali na tumekuwa tukifanyia kwa vitendo yale tunayoyasoma na kwa hakika vimetuzalia matunda".

Naye Delfina Uromi anasema kuwa, kupitia jarida la *Mkulima Mbunifu* tumejifunza madhara ya sumukuvu na namna ya kujikinga nayo toka mazao yakiwa machanga, kitu ambacho hapo awali hatukuwa tunafahamu na tumekula sana sumu kuu kupitia mazao mbalimbali kwani hatukuwa na uelewa.

Tumejifunzaji pia kuhusu gugukaroti, gugu ambalo hatukuwa tunafahamu kama ni sumu, tulilichukulia tu kama magugu mengine ya kawaida na hata mifugo ilikuwa ikila kama malisho, ila kwasasa tumefahamu madhara yake na namna ya kulidhibiti.

Aidha, tumejifunza kuhusu ufugaji wa kuku, magonjwa na namna ya kudhibiti na kuwapa kuku chanjo, lakini pia kuhusu mpera ambao utupatia matunda, faida za majani ya mpera na namna ya kutumia kutibu magonjwa mbalimbali ya binadamu. Alisema Delfina.

Naye Joyce Kimario aliongeza kuwa, kupitia jarida la *Mkulima Mbunifu*, nimejifunza kuhusu kilimo cha bamia, karoti na mbogamboga lakini pia nimeweza kuzalisha kwa kusoma na kufanya kwa vitendo.



Mmoja wa wanakikundi Bi. Genofeva Asenga akionyesha unga wa ndizi kitarasa bidhaa inayotengenezwa na wanakikundi wa Mangulwa Earth Market

Aidha, nimeweza kujifunza namna ya kuzalisha mbolea ya mboji, kutengeneza dawa za asili kwa kutumia malighafi mbalimbali kama vile kitunguu saumu, pilipili, majani ya mpapai, sabuni na hivyo kuondokana na tatizo la magonjwa katika shamba langu.

Changamoto

Waswahili wanasema "penye mafanikio hapakosi changamoto", hivyo pamoja na mafanikio wanakikundi hawa pia wanakutana na changamoto mbalimbali katika uzalishaji ambapo wameweza kubainisha na kuomba kama kuna namna wanaweza kusaidika katika kutatua.

Wanakikundi hawa wamesema kuwa, changamoto kubwa ni mabadiliko ya hali ya hewa, yaani kupungua kwa mvua au wakati mwingine kutokunyeshwa kwa wakati jambo ambalo linapelekea kushindwa kwa uzalishaji.

Aidha, ukosefu wa malisho, magonjwa mbalimbali ya mimea hasa ugonjwa ma migomba, magonjwa ya mlipuko kwa mifugo kama kuku pamoja na ukosefu wa masoko hasa wakati ambapo mavuno yanakuwa mengi kama uzalishaji wa ndizi.

Wito kwa Mkulima Mbunifu

Wakulima hawa wanaomba kuendelea kupokea majarida ya *Mkulima Mbunifu* na kuwezesha kwa njia zingine ikiwa ni pamoja na elimu kwa vitendo ili kuweza kusonga mbele zaidi katika kujikumu kimaisha na kiuchumi kwa ujumla.


Vuruga biocide: Kiutilifu cha asili sasa chapatikana kwa ruzuku

Hayawi hayawi sasa yamekua. Mvumilivu, hula mbivu. Ni muda wakulima wa kilimo hai wamekua wakilalamika upatikanaji wa bidhaa za kilimo hai kwa urahisi. Serikali ya Tanzania kupitia wizara ya kilimo imepitisha kiutilifu hai kwa jina la Vuruga.

Erica Rugabandana

Kiutilifu hai (*VURUGA BIOCIDES*) kimetengenezwa kwa vimelea asili vya fangas (*A. oryzae*) kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya mazao shambani hasa jamii ya vipepeo (*Moth*). Pia kimefanyiwa majaribio kwa muda mrefu katika mikoa mbalimbali Tanzania katika kudhibiti wadudu wasumbufu wengi ikiwemo; Kanitangaze, viwavi jeshi vamizi, viwavi wanaoharibu pamba, viwavi wanotoboa matunda (maembe) na mbogamboga kama mchicha, mnavu, chainizi, kabichi na pamba.

Kiutilifu hiki pia kimetengenezwa katika mifumo mingi inayoweza kutatua changamoto za usugu wa visumbufu.



Vuruga Biocide (VB) inafaa kutumia katika mazao ya nyanya, viazi, mahindi na mboga mboga, maua na pamba kuanzia wiki ya tatu tangu mimea kuoteshwa.

Namna ya kutumia kiutilifu cha vuruga

Pima mililita 2 changanya na lita 1 ya maji safi, nyunyiza kwenye majani, shina au matunda. Pima kwanza maji nusu kwenye pampu kisha weka kiutilifu katika uwiano unaostahili, malizia kiasi cha maji kilichobaki kukamilisha ujazo wa pampu. Kisha nyunyiza kwenye majani machanga ya mimea au maua au matunda machanga ili kudhibiti wadudu wanaotarajia kuharibu matunda kabla ya kukomaa. Nyunyiza kiutilifu nyakati za jioni kuanzia saa 11 jioni kwa ufanisi wa hali ya juu. Nyunyiza kiutilifu upande wa chini ya majani au kwenye funeli ya mhindi na tumia



pampu sahihi yenye nozo ya wadudu yenye matundu madogo zaidi (inayotoa maji kama mvuke). Hifadhi sehemu ya utulivu nyuzi joto isiyozidi 30, weka mbali na watoto na hifadhi mbali na jua/mwanga kwa matokeo mazuri zaidi.

Matokeo ya vuruga katika majaribio katika mazao

Kiutilifu hiki (*VURUGA BIOCIDES*) kimefanyiwa majaribio tangu 2016

Faida zake

- Ni cha asili (*Organic*),
- Hutengenezwa kwa malighafi zinazopatikana nchini
- Ni salama kwa binadamu, wadudu rafiki na mazingira
- Ina ufanisi kwa asilimia 90-100
- Huangamiza visumbufu vingi sugu vya mazao hasa Kanitangaze, viwavi jeshi, wadudu wa pamba, chawa jani, viwavi wa pamba nk.
- Kinapatikana kwa gharama nafuu ukilinganisha na viuatifu vingine
- Kinafanya kazi tatu kwa mpigo: mbolea, kiutilifu na huvuta wadudu rafiki katika mimea
- Si rahisi kujenga usugu kwa wadudu, ni suluhisho la kudumu (*sustainable*)

Katika jitihada za serikali kuhakikisha mkulima anazalisha mazao salama, ilikulinda afya ya mmea na mlaji, pia kuzingatia uendelevu kiutilifu hiki sasa kinapatikana kwa ruzuku. *Mkulima Mbunifu* imeshuhudia ugawaji wa kiutilifu hiki kwa wakulima wilayani Babati, Mkoani Manyara.

hadi sasa katika mikoa ya Mbeya, Arusha, Manyara, Morogoro, Manyara, Dar es salaam, Pwani, Iringa na Simiyu katika kudhibiti visumbufu jamii ya viwavi; Kanitangaze na viwavi jeshi vamizi, viwavi wa pamba, chawa jani nk.



Afisa kilimo Babati, Bi Florence Mkome (Kushoto) akitoa maelezo juu ya utumiaji wa kiutilifu hai wakati wa ugawaji wa kiutilifu cha Vuruga Biocide katika kijiji cha komoto

MKUTANO MKUU WA PILI WA KILIMO IKOLOJIA AFRIKA MASHARIKI

Kutumia Uwezo wa Kilimo Ikolojia katika Kubadilisha na Kudumisha Mifumo ya Kilimo na Chakula

MADA:

Kuimarisha Mabadiliko ya Mfumo wa Kilimo na Chakula kwa Ustahimilivu, Uendelevu na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi

Wasiliana nasi:

www.ea-agroecologyconference.org
info@ea-agroecologyconference.org

[f](#) [X](#) [in](#) Biovision Africa Trust

For More details Scan the QR Code



25 - 28 Machi 2025

Argyle Grand Hotel
Nairobi Kenya



Kutumia Uwezo wa Kilimo Ikolojia katika Kubadilisha na Kudumisha Mifumo ya Kilimo na Chakula



Msomaji wa jarida la MkM atoa ushauri kwa wafugaji wa kuku

Moja ya kazi inayofanywa na Mkulima Mbunifu katika kufikisha elimu kwa wakulima, ni kutumia ujuzi na uzoefu wa wakulima na wafugaji wengine katika kuelimisha na kushirikisha namna mbalimbali wanavyofanya na kufanikiwa katika kazi zao za uzalishaji.

MkM

Huu ni ushauri kutoka kwa mmoja wa wasomaji wa jarida la Mkulima Mbunifu kwa wafugaji wa kuku.

“Naitwa Nicodemus Nzenga, ni mmoja kati ya wasomaji wazuri wa jarida lenu. Nashukuru na kuwapongeza, kwani jarida linaelimisha na kutoa mbinu mbadala za kuinua maisha ya wakulima wadogo.

Mimi ni mfugaji mdogo wa kuku wa asili mwenye uzoefu wa kiasi wa shughuli hizi. Nadhani haitakuwa vibaya nikitumia muda huu kubadilishana mawazo na wafugaji wenzangu kuhusu vifo vya vifaranga na nini kisababishi?”

Ufugaji holela: Vifaranga wanatumia muda mrefu kukimbizana na mama yao kutafuta chakula na hivyo kupata misukosuko mingi kama ajali, wanyama, ndege na hata kupotezana na mama yao.

Suluhisho: Wafungwe katika chumba maalumu au wapumzishwe kadri inavyowezekana kwani hata chakula wanachopata wanakitumia kutembea na kukimbizana na mama yao badala ya kujenga miili yao.

Magonjwa: Vifaranga wanapotolewa tu huambukizwa magonjwa kwani hukumbana na maeneo ambayo tayari yalishachafuliwa na kuku wakubwa. Mbaya zaidi ni kwamba kuna magonjwa ambayo wanaweza kutoka nayo katika yai hivyo huwachukua wiki mbili tu na kuanza kufa.

Suluhisho: Viranga wapewe antibiotics ndani ya siku saba za uhai wao ili kuepuka magonjwa ya bakteria.

Ikumbukwe kwamba uwezo wa kuku wakubwa kuvumilia magonjwa ni mkubwa kuliko wa vifaranga, hivyo wakifugwa pamoja vifo hutokea kwa magonjwa na hata kuuwawa na kuku wakubwa/majogoo wasiopenda vifaranga.

Suluhisho: Ni vyema viranga wakatengwa na kuku wakubwa.

Upungufu wa vitamin A: Hili ni tatizo kubwa hasa wakati wa kiangazi ambapo hakuna uoto wa kutosha na pia uwezo wa vifaranga kula majani ni mdogo hivyo vifo vingi vinatokea kwa upungufu wa vitamin A bila hata ya kuonyesha dalili yoyote.

Suluhisho: Vifaranga waanze kupewa Vitamin A siku ya kwanza kwa kufuata maelezo ya watengenezaji wa vitamin hiyo.

Wadudu: Utitiri, viroboto na wadudu wengine washambuliao kuku viranga hutotolewa na kukumbana na wadudu hao toka siku ya kwanza



tu na unaweza ukakuta wengine wanashindwa kutoa hata sauti na vifo hutokea.

Suluhisho: Kuku wanapoanza kuhatamia waandaliwe kwa kuwekewa viota safi na dawa za kuua wadudu hao ili vifaranga watotolewe katika mazingira safi yasiyokuwa na wadudu hao.

Unyevu: Kuku anaweza akakumbatia vifaranga wake lakini chini kukawa na unyevu au baridi hivyo lengo la kuvipatia joto halitatimia.

Suluhisho: Hakikisha banda ni safi na halina unyevu wala uchafu wa aina yoyote ile.

Nicodemus Nzenga, Msimamizi wa Upendo nyuki group,
niconzengatz2@gmail.com



mkulimambunifu.org,
theorganicfarmer.org
infonet-biovision.org

+255 717 266 007

http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu

http://twitter.com/mkulima_mbunifu

https://www.instagram.com/mkulima_mbunifu

